**KISWAHILI DARASA LA NNE**

**LUGHA MUHULA WA KWANZA**

**SURA YA KWANZA**

**Ufahamu: urafiki wa paka na panya**

- Kuchambua picha
- Kuorodhesha msamiati na kueleza maana yake
- Kutunga sentensi kwa kutumia msamiati
- Kusoma ufahamu
- Kuchambua msamiati ibuka

Tathmini: mufti uk 2-3

**Sarufi: ngeli ya A-WA na viashiria**

Ngeli ni vikundi maalum vya majina au nomino kulingana na sifa Fulani

Mifanio ya ngeli za A-WA ni nomino na wanadamu, wanyama, wadudu, samaki na nyuni

Viashiria ni maneno yanayoonyesha alipo mtu au kilipo kitu

Ni vya aina tofauti

- Viashiria vya karibu huyu—hawa
- Mbali kidogo huyu—hao
- Mbali sana Yule—wale

Wanafunzi wasome mifano na kutazama michoro

Tathmini: mufti uk 3-6

Kurunzi uk 7-8

Kkd uk 8

**Kusikiliza na kuongea**

**Maamkizi , adabu na heshima**

Maamkizi na salamu ni kujuliana hali kati ya watu wakutanapo

Huonyesha adabu na heshima aliyo nayo mtu kwa wengine

Mifano

- Habari za asubuhi — njema, nzuri
- Hujambo — sijambo
- Shikamoo — marahaba
- Waambaje — sina la kuamba

Mfano wa maneno ya adabu

- Pole
- Asante
- Nashukuru
- Simile
- Samahani
- Naomba
- Tafadhali
- Endesha
- Mjamzito

Tathmini: mufti uk 8

Kurunzi uk 12-13

Kkd uk 3

**Kuandika**

**Uakifishaji: insha**

Mwalimu ayataje mambo muhimu ya kuzingatiwa

Mfano:

- Herufi kubwa
- Koma
- Kituo
- Hisi
- Kishangao
- Kiulizi

Tathmini: mufti uk 8

Kurunzi uk 9

Kkd uk 14

**Msamiati: jikoni**

Jikoni ni pahali pa kupikia vyakula mbalimbali

Mwalimu awashilikishe kusoma chati,

kutazama mifano

- Seredani
- Chano
- Mbuzi
- Kinu na mchi
- Uteo
- Buli
- Birika
- Buli
- Birika
- Bilauri

Mwalimu awashilikishe kutoa mifano zaidi

Tathmini: mufti uk 10

Kurunzi uk 3-4

**SURA YA PILI**

**Kusoma: shairi**

**Haki za watoto**

Kuchambua msamiati husika katika shairi

Mfano:

- Ubeti
- Mshororo
- Malenga
- Manju

Kuchambua picha

Kuwashirikisha kughani shairi kwa vikundi ,mmojammoja

Tathmini: mufti uk 13

**Sarufi:**

**Ngeli ya A-WA NA VIULIZI**

Ngeli ni vikundi maalum vya nomino au majina

Ngeli za A-WA ni nomino na wanadamu, wanyama, wadudu, samaki , nyuni na mauti

Viulizi ni maneno ya kuulizia kwa nia ya kujua zaidi

Viulizi ni –pi?, -ngapi? na –gani?

Tathmini: mufti uk 15-16

Kurunzi uk 14-15

Kkd uk 4

**Kuandika: sentensi**

Sentensi zenye koma na kikomo

Matumizi ya koma: kuorodhesha vitu

KamaKipumuo

Kikomo: mwisho wa sentensi

Mfano: mama alinunua sukari, chumvi, unga na wimbi.

Ninacheka.

Tathmini: mufti uk 18

**Kusikiliza na kuongea**

Sentensi zenye vitate

Vitate ni vitatanishi. Yaani maneno yanayotatanisha kimatamshi

Hukaribiana kimaandishi lakini hutofautiana kimatamshi na maana

Mfano:

- Tai tia
- Tua tuma
- Juma chuma
- Jenga chenga
- Dona damu

Motto mwenye adabu hakupewa adhabu

Yule mjusi mjuzi aliangukia mchuzi

Baba mwenye papa anadai tai yake

Tathmini: mufti uk 17

Kurunzi uk 17

Kkd uk 20

**Msamiati: shambani**

Shambani ni mahali pa shughuli za kukuza mimea

Shughuli hizi ni kama:

- Kufyeka
- Kuruna
- Kupalilia
- Kulima
- Kupanda
- Kupiga dawa
- Kunyunyizia maji
- Kupiga matuta

Kutaza michoro na kuchambua huku wakisoma maelezo

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kuigiza baadhi ya vitendo

Tathmini: mufti uk 21-22

Kurunzi uk 13-14

Kkd uk 16-17

**SURA YA TATU**

**Kusoma: ufahamu**

Karamu ya kaka Abedi

- Kuchambua picha
- Kuchambua na kueleza maana ya msamiati
- Kutunga sentensi kutumia msamiati husika
- Kusoma ufahamu na kuchambua msamiati ibuka
- Kueleza kwa kifupi

Tathmini: mufti uk 6

**Sarufi:**

**Ngeli ya U-I na viashiria**

Nomino katika ngeli hii huchukua viambishi M, MW au MU katika umoja na MI katika wingi

| | | |
|---|---|---|
| Viashiria ni: | huu | hii |
| | Huo | hiyo |
| | Ule | ile |

Mfano:

- Mpira ule umepatikana — mipira ile imepatikana
- Mkono huu unauma — mikono hii inauma
- Msitu huo una wanyama — misiyu hiyo ina wanyama

Tathmini: mufti uk 25-26

Kurunzi uk 18-19

Kkd uk 55

**Kusikiliza na kuongea**

Sentensi zenye maneno tate

Kuwashirikisha kueleza vitate

Kuwashirikisha kutoa jozi za vitate

Mfano:

- Toa — doa
- Papa — baba
- Pipi — bibi
- Basi — pasi

Kuwashirikisha kusoma sentensi

Tathmini: mufti uk 27

Kurunzi uk 23

Kkd uk 31

**Msamiati:**

**Maumbo**

Kutazama mchoro na kuchambua maumbo

Kuchambua majina ya maumbo

Kutaja maumbo na kuyachora

Kusoma maelezo kuhusu maumbo

Mifano

- Pia
- Mraba
- Mcheduara
- Pembetatu

Tathmini: mufti uk 28

Kurunzi uk 23

Kkd uk 33

**Kuandika**

**Alama ya hisi**

Kishangao au hisi hutumika kuonyesha hisia za mneneji

Hisia zaweza kuwa za furaha, huzuni, mshangao, nk

Hisi hutumika sana baada ya kihisishi na hufuatwa na herufi kubwa kama ni katikati ya sentensi

Mfano:

- Ala! Kumbe ni mwizi!
- Hoyee! Tumeshinda!
- Kumbe Omura ni pwagu!

Tathmini: mufti uk 27

Kurunzi uk 42,123

Kkd uk 175

**SURA YA NNE**

**Kusoma: ufahamu**

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kuwashirikisha kusoma

Kuchambua msamiati ibuka

Tathmini: mufti uk 31

**Sarufi**

**Ngeli ya U-I na viulizi**

Viulizi ni maneno yanayotumika kujua idadi

Navyo ni:

- -pi?
- -ngapi?
- Gani?

Mfano

| | |
|---|---|
| Mkono upi unauma? | Mikono ipi inauma? |
| Mti gani utakatwa? | Miti gani itakatwa? |
| Milima mingapi ina theluji? | |

Tanbihi: kiulizi ngapi? Hakitumiki kwa umoja

Tathmini: mufti uk 35-36

Kkd uk 14

**Kusikiliza na kuongea**

**Vitendawili**

Kuwaongoza kutoa utangulizi

Kuorodhesha utangulizi

Kuwapa mifano

Kuwapa fursa kutegeana vitendawili

Mfano wa utangulizi

Mtegaji: kitendawili

Mtegewa: tega

Sahani

Ya mchele

Tathmini: mufti uk 29

Kurunzi uk 41

Kkd uk 69

**Msamiati**

**Magonjwa/ maradhi/ ndwele**

Ugonjwa ni hali inayompata mtu baada ya kuadhiriwa na riini

Kutaja magonjwa

Kuchambua msamiati

Kusoma maelezo na kuchambua msamiati ibuka

Tathmini: mufti uk 35

Kurunzi uk 37

Kkd uk 34

**Kuandika**

**Kiulizi**

Kiulizi ni alama itumikayo mwishoni mwa sentensi kuulizia swali (?)

Mifano

Je, unatoka wapi?

Unamjua mwalimu bokono?

Nani alimchokoza Rashid?

Kiazi gani kinaliza?

Tathmini: mufti uk 37

Kurunzi uk 42

Kkd uk 175

**SURA YA TANO**

**Kusoma: magazeti**

Kuchambua mada

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati husika

Kusoma maelezo na kuchambua msamiati ibuka

Kujadiliana

Tathmini: mufti uk 41

Kurunzi uk 42

Kkd uk 142

**Sarufi**

**Ngeli ya KI-VI pamoja na viashiria na viulizi**

Viulizi ni maneno ya kujulia au kuulizia swali

Ngeli hii huchukua kiambish KI kwa umoja na VI kwa wingi

Mfano

- Kiazi kile ni change viazi vile ni vyetu
- Kiatu chake ni kipi? Viatu vyao ni vipi?
- Kile ni kikapu vile ni vikapu
- Kinu gani kinatwangiwa nafaka?

Tathmini: mufti uk 44-45

Kurunzi uk 26

Kkd uk 163

**Kusikiliza na kuongea**

**Mzee ndovu na kaka sungura**

Kuchambua picha

Kuorodhesha msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi kutumia msamiati

Kuwashirikissha kusoma

Kuchambua msamiati

Tathmini: Kkd uk 175

**Kuandika**

**Sentensi**

Kusoma sentensi

Kuwaongoza kueleza alama ya uakifishaji na matumizi yake

Kuwashirikisha kutambua alama zilizotumika

Kunakiri sentensi madaftarini

Mfano

Mkono wangu ulichafuka nikaunavya

Tathmini: mufti uk 46

**Msamiati**

**Alama na ishara za barabarani**

Kutazama alama hizo

Kuchambua michoro na misamiati

Kusoma maelezo

Kutoa maana

Kuchora na kutoa maelezo

Tathmini: mufti uk 48

Kurunzi uk 45

Kkd uk 46

**SURA YA SITA**

**Kusoma ufahamu**

Mnara wa Baberi

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati husika

Kutunga sentensi kutumia msamiati huo

Kushiriki usomaji

Kuchambua msamiati ibuka

Tathmini: mufti uk 53

**Sarufi**

**Ngeli LI-YA**

Nomino huchukua kiambishi LI kwa umoja na YA kwa wingi

Nomino huwa

- za kawaida

Huchukua MA au ME kwa wingi

- Za ukubwa

Mifano

| | | | |
|---|---|---|---|
| ❖ Jiwe | mawe | ❖ Jumba | majumba |
| ❖ Jino | meno | ❖ Jitu | majitu |
| ❖ Zulia | mazulia | ❖ Lango | malango |
| ❖ Jambo | manmbo | ❖ Guu | maguu |
| ❖ Bwawa | mabwawa | ❖ Toto | matoto |
| ❖ Jiko | majiko | ❖ Buzi | mabuzi |

Tathmini: mufti uk 55-59

Kurunzi uk 86

Kkd uk 37

**Kusikiliza na kuongea**

**Hadithi**

Kuchambua utangulizi

Kuwapa fursa kutamba hadithi

Mfano wa utangulizi:

Msimulizi: paukwa

Wasikilizaji: pakawa

Msimulizi: paliondokea chanjagaa….

Chambua mambo muhimu ya kuzingatiwa- urefu, lugha

Tathmini: risa ya wanafunzi

**Kuandika**

**Hati nadhifu**

Hati ni mwandiko

Mwandiko sharti uwe nadhifu

Uwaongoze kusoma sentensi

Kuchambua alama za uakifishaji zilizotumika

Kuwaongoza kuandika kwa hati nadhifu

Kuwashirikisha kusoma sentensi

Tathmini: mufti uk 60

Kurunzi uk 32

Kkd uk 144

**Msamiati**

**Wanyamapori**

Kutazama michoro

Kuchambua msamiati husika

Kusoma maelezo na kuchambua msamiati ibuka

Kutazama picha

Kuchora baadhi ya wanyama na kutoa sifa zao

Mfano

Samba ni mkali

Tathmini: mufti uk 60

Kurunzi uk 61

Kkd uk 75

**SURA YA SABA**

**KUSOMA: UFAHAMU**

Ajabu ya Jongoo

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati mhusika

Kutunga sentensi kutumia msamiati

Kusoma ufahamu

Kutambua msamiati ibuka na kuchambua

Tathmini: mufti uk 65-66

**Sarufi**

**Nafsi**

Kunazo nafsi tatu

- Nafsi ya kwanza MIMI SISI
- Nafsi ya pili WEWE NYINYI/ NINYI
- Nafsi ya tatu YEYE WAO

Viwakilishi ni maneno yanayochukua nafasi ya neon

Viwakilishi vya nafsi ni:

| nafsi | Viwakilishi | |
|---|---|---|
| | umoja | Wingi |
| Mimi/ sisi | ni | Tu |
| Wewe/ nyinyi | u | M |
| Yeye/ wao | a | Wa |

Mifano

- Mimi ni mwanafunzi
- Ninasoma
- Nyinyi ni wema
- Wanakimbia

Tathmini: mufti uk 67

Kurunzi uk 46

Kkd uk 20,26,44

**Kusikiliza na kuongea**

**Semi**

Semi ni utungo au muungano wa kitenzi na nomino za kawaida kuleta maana maalum fiche

Kutumika kuelimisha, kuonya na kuburudisha

Mifano

- Piga mbio kimbia
- Enda mrama haribika
- Kata kamba kufa
- Ona haya fedheheka
- Kata kiu kunywa maji
- Shtaki njaa kula
- Enda shoti kimbia

Tathmini: mufti uk 105

Kurunzi uk 97

Kkd uk 50

**Kuandika**

**Alama ya kistari kifupi**

Hutumika kuonyesha kwamba neon limekatwa

Kwamba halijakamilika upande wa kulia

Mfano

Mama alienda sokoni akanunua mboga, karoti, parachi-

Chi na mihogo

Tanbihi: usitenganishe silabi

Tathmini: mufti uk 70

Kkd uk 175

**Msamiati: ukoo**

Ukoo ni watu wenye uhusiano wa karibu kwa damu au ndoa

Mfano

- Nina/ mama
- Baba
- Babu
- Nyanya/bibi
- Dada
- Kaka
- Mnuna
- Mjomba/hau
- Shangazi
- Motto/mwana
- Binamu
- Babu mkuu
- Mama wa kambo
- Mpwa
- Mkazamwana
- Halati/ hale
- Ami/ amu
- Kitukuu

Kuwashirikisha kutazama michoro na kusoma maelezo

Kuigiza

Tathmini: mufti uk 72

Kurunzi uk 74

Kkd uk 80

## SURA YA NANE

**Kusoma : shairi**

Shairi ni wimbo wa Kiswahili

Huwa na sheria tunazoita kanuni za ushairi

- Ubeti: kifungu cha mishororo
- Mshororo: msatri katika ubeti
- Malenga: mtunzi wa mashairi
- Manju: anayeghani/ anayekariri shairi

Kuwashirikisha kusoma shairi

Kuwashirikisha kughani kwa sauti

Kuchambua msamiati

Tathmini: mufti uk 75

**Sarufi**

**Nafsi na nyakati LI na TA**

Nafsi tatu

| nafsi | umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1 | Mimi | Sisi |
| 2 | Wewe | Nyinyi |
| 3 | yeye | wao |

LI: huonyesha wakati uliopita

Hukanushwa kwa KU

MFANO:

- Nilisema sikusema
- Alienda hakuenda
- Ulicheka hukucheka

NA :huonyesha wakati uliopo

Kwa ukanusho NA hutoweka

Mfano

| | |
|---|---|
| Ninachora | sichori |
| Tunalima | hatulimi |
| Unaimba | hatuimbi |
| Mnasimama | hamsimami |
| Anasema | hasemi |
| Wanasema | hawasemi |

Tanbihi: irabu ya mwisho hugeuka na kuwa i

Washirikishe kusoma jedwali

Tathmini: mufti uk 77

Kurunzi uk 62

Kkd uk 20,26

**Kusikiliza na kuongea**

**Shairi: Adabu**

Shairi ni wimbo wa Kiswahili

Shairi hughaniwa na kukaririwa na mtu mmoja au zaidi

Kusoma shairi

Kuchambua msamiati

Kughani katika vikundi

Tathmini: mufti uk 78

**Kuandika**

**Barua ya kirafiki**

Kuandikiwa watu wa ukoo au rafiki

Kueleza sehemu

**Anwani**: huwa ya mwandishi

Huonyesha

- jina la mwandishi au shule
- Sanduku la posta
- Mji
- Terehe
- Utangulizi: mfupi na unaovutia
- Kiwiliwili: mwili huonyesha madhumuni ya uandishi
- Mwisho: hutoa ujumbe wa mwisho kwa muhtasari
- Wasalaam/ maagano

Huaga mwandikiwa

Huonyesha uhusiano uliopo baina ya mwandishi na mwandikiwa

Mfano:

- Mwanao mpendwa
- Refikiyo wa dhati

ANWANI

TAREHE

UTANGULIZI

MWILI/ KIWILIWILI

WASALAAM/ MAAGANO

**Msamiati**

**Ndege/ nyuni**

Nyuni ni viumbe wenye manyoya

Huruka hewani kwa mbawa

- Mdomo wa ndege ni vidona
- Makanyagio ni makacha
- Paja la ndege ni kiga

Ndege huishi kwa kiota

Nyuni wa mwituni huishi kwa mwitu/ msitu/ porini

Hawafugwi nyumbani

**Baadhi ya nyuni ni:**

- Korongo
- Kipanga
- Heroe
- Mbayuwayu
- Sigi
- Mwewe
- Koho
- Kanga
- Ninga
- Kasuku
- Mbuni
- Kunguru
- Kongoti
- Tausi

Tathmini: mufti uk 95

Kurunzi uk 85

Kkd uk 83

**SURA YA TISA**

**Kusoma ufahamu**

Maombi matatu(2)

Kurejelea sehemu ya kwanza

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati husika

Kutunga sentensi kutumia msamiati

Kushiriki usomaji

Tathmini: mufti uk 86-87

**Sarufi**

**Nafsi pamoja na nyakati TA na HU**

Kuna nafsi tatu

TA: huonyesha wakati ujao

HU: huonyesha wakati wa mazoea

Mfano

- Nitasoma sitasoma
- Utasoma hutasoma
- Atasoma hatasoma

HU

- Husoma(mimi) sisomi
- Husoma(wewe) husomi
- Husoma(yeye) husomi
- Husoma(mimi) hatusomi
- Husoma(wewe) hamsomi
- Husoma(yeye) hawasomi

Kusoma jedwali

Tathmini: mufti uk 89-90

Kurunzi uk 62

Kkd uk 44

**Kusikiliza na kuongea**

**Nyimbo**

Wimbo ni utungo wenye mapigo maalum na mahandhi

Washiriki uimbaji katika vikundi

Kuchambua mambo muhimu ya kuzingatiwa

Tathmini: uimbaji wa wanafunzi

**Kuandika**

**Sentensi**

Sentensi huundwa kwa maneno yenye mpangilio maalum

Kujadili aina za maneno – nomino vitenzi, vivumishi na vielezo

Kuwashirikisha kusoma

Kuwaongoza kutambua maneno na kuyapanga

Tathmini: mufti uk 90-91

Kurunzi uk 87

**Msamiati**

**Rangi**

Rangi za upinde wa mvua

Upinde wa mvua ni alama yenye michoro ya rangi tofauti inayoonekana kuonyesha na kuna miale ya jua

Upinde wa rangi tofauti saba na hufuata kama:

- Nyekundu
- Machungwa
- Manjano
- Kijani
- Samawati
- Nili
- Urujuani

Tathmini: mufti uk 92

Kurunzi uk 99-103

Kkd uk 93-94

**SURA YA KUMI**

**MARUDIO**

Kusoma

Matamshi

Maneno:

Kusoma maneno kwa ufasaha

Sentensi:

Kuchambua maneno

Kusoma sentensi

**Kuandika**

**Hati**

Hati ni mwandiko

Sharti uwe nadhifu na herufi zichongwe ipasavyo

Kuandika sentensi kwa hati nadhifu

Tathmini: mufti uk 94

**Kusikiliza na kuongea**

**Tanakali**

Sauti huigwa na kutamkwa

Hufuatwa na hisi

Mfano

- Maji yalimwagika mwa!
- Kuna giza totoro!
- Mwizi alipigwa akafa fofofo!

**Vitendawili**

Utungo unaohitaji kuteguliwa

Huwa na anayetega : hutoa swali

Mtegewa hutoa jibu

Jibu likikosekana mtegaji hupewa mji

Mfano

- Askari mlangoni: kufuri
- Mzee mwenye kabuti la chuma: kombe

**Methali**

- Mtaka yote hukosa yote
- Motto wa nyoka ni nyoka

Tathmini: mufti uk 95

Kurunzi uk 69,29

Kkd uk 127

**Sarufi**

**Ngeli**

Kujadili ngeli

- Milango U-I
- Yai LI-YA
- Kuku A-WA

Wingi

- Mimi ninakula chakula kitamu
- Sisi tunakula vyakula vitamu

Tathmini: mufti uk 96-97

**Msamiati**

Jadili msamiati tofauti

Mwalimu aulize maswali ya kauli, wanafunzi wasikilize na wayajibu

Kuwashirikisha kutaja msamiati tofauti na kujadili mifano tofauti

Kuwauliza waeleze mbele ya wenzao

Kuwapa maswali ya lugha mseto ubaoni

**Msamiati:**

- Tarakimu
- Jikoni
- Magonjwa
- Wayama pori
- Ukoo
- Vikembe

Tathmini: mufti uk 98

Kkd uk 192-225

# INSHA

## RAFIKI YANGU

Rafiki ni mtu umpendaye

Huwa mna uhusiano mzuri na wa karibu

Rafiki pia huitwa sahibu, muhibu au mwendani

**Msamiati**

Jina lake

Umri alio nao (miaka)

Darasa na shule yake

Wazazi/ wavyele wake na kazi zao

Rangi ya ngozi yake

Urefu, umbo

Ndugu zake

Masomo apendayo

Michezo aipendaye

Chakula/ mlo aupendao

Mambo/ shughuli mtekerekazo pamoja

Hukusaidia vipi

Kwanini unampenda

**Mapambo**

Rafiki yangu ana nywele nyeusi tititi na ndefu kama sinya ya samba

Meno meupe pepepe

Macho madogo na mazuri kama ya malaika

Huwa safi na nadhifu

Mfupi kama nyundo/ mbilikimo

Nina yake ni mkufunzi na baba yake ni daktari/ tabibu

Mnuna wake huitwa

Ana urefu wa wastani

Hupenda somo la sayansi, Kiswahili, hisabati

Hupenda kucheza kandanda

Hupenda kula wali kwa kitoweo cha nyama

Hunywa sharubati, maji, soda au chai ili kukonga roho

Sisi hucheza pamoja, kusoma hadithi, kutembelea wakongwe na kuwasaidia wavyele

Sisi husaidiana shuleni

Laazizi hunisaidia kwa masomo na kufanya uamuzi wa mambo maishani

**Tashbihi**

Eupe kama theluji

Eusi kama makaa/ mpingo

Mnene kama nguruwe

Mwaminifu kama mchana

Msiri kama kaburi/ usiku wenye kiza

**Methali**

Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu

Akili ni mali

Ukiona vyaelea jua vimeundwa

Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu

## SHULE YETU

Jina

Lilianzishwa na nani

Mkuu wa shule ni nani

Idadi ya wakufunzi na wanagenzi

Wafanyikazi wengine

Mijengo na majengo yaliyopo

Shamba/ konde/ mgunda- mimea mkuzayo na wanyama mfugao

Mna mabasi mangapi

Mandhari ya shule-miti/ maua

Mazingira yenyewe

Wafanyikazi ni kv. Wapishi, madereva, mabawabu, muuguzi, sekretari

Mijengo dhabiti na imara. Imejengwa kwa mawe na waashi stadi

Kuna majengo kama:

- Bwado: chumba cha maakuuli/ mlo
- Bweni: vyumba vya kulala
- Maktaba: kuhifadhi vitabu na majarida
- Maabara: uchunguzi wa kisayansi
- Choo
- Madarasa
- Majilisi: walimu hufanya maandalizi na masahihisho
- Hamamu/ bafu: kuogea
- Boma: zizi, zeriba-ngombe
- Ghala/ stoo: kuhifadhi mazao baada ya kuvuna
- Jikoni: shughuli za mapishi

Mimea kama:

- Mahindi
- Mipareto
- Miparachichi
- Mikahawa
- Miboga
- Michungwa

Wanyama tufugao kama:

- Ngamia
- Nguruwe
- Bata
- Ninga
- Ng'ombe
- Kondoo
- Kuku
- Kasuku
- Mbuzi
- Kelbu

Mabasi matano yafananayo kama shilingi kwa ya pili

Kuna miti mirefu na mifupi na maua mazuri

Mazingira nadhifu na safi

Masomo kama sayansi, king'eng'e, Kiswahili, dini, somo la jamii, tarakilishi, kifaransa na hisabati

Michezo kv: kandanda, jugwe, voliboli, mpira wa vikapu

**Tashbihi**

Fanana kama shilingi kwa ya pili

Miti mirefu kama unju/ mlingoti

Waaminifu kama mchana

Nukia kama ruhani

Metameta kama nyota angani

**Methali**

Elimu ni bahari

Mwenye macho haambiwi tazama

Motto umleavyo ndivyo akuavyo

## UMUHIMU WA MITI

Mti ni nini

Sehemu zake

Manufaa

Mti ni mmea wenye shina, mizizi, matawi, tanzu, maua na matunda

Mti mdogo ni mche-miche

Mbegu huota- huchipuka na kunawili

**Manufaa**

Hutupa mbao-seremara huunda samani/ fanicha

Hutupa chakula- matunda hutupa vitamin mwilini na hutukinga dhidi ya magonjwa

Hutengeneza nyua-mipaka

Huzuia mmomonyoko wa udongo

Hutupa kivuli wakati wa kiangazi

Huvuta mvua-hutupa maji

Makao ya hayawani wa mwituni na nyuni

Huzuia/ hukinga upepo mkali

Vyakula vya wanyama-majani

Chanzo cha mito na chemichemi za maji

Hutupa makaa na kuni-yatumikayo kwa upishi

Vikingi na fito-ujenzi

Kutengeneza karatasi na penseli

Kutengeneza gundi

Hutupa dawa za kiasili/ kienyeji

**Tashbihi**

Miti mirefu kama unju/ mlingoti

Maua hunukia kama ruhani

Hupendeza kama bibiharusi

**Methali**

Mti ukifa sinare na tanzuze hukauka

Mti mkuu ukigwa wanandege huyumba

Maji ni uhai

Mtaka cha mvunguni sharti ainame

Ukikata mmoja panda miwili

Penye miti hapana wajenzi

Tusikate miti ovyo ardhi itakuwa jangwa

Miti mingi pamoja huwa msitu, mwitu au pori

## BARUA YA KIRAFIKI

Huandikiwa watu wa ukoo au sahibu

Mwandishi na mwandikiwa huwa na uhusiano wa karibu

Lugha huwa sanifu

Sehemu zake ni:

**Anwani**

Huwa moja tu ya mwandishi

Huwa na :

- Jina la mwandishi
- Sanduku la posta
- Mji

**Tarehe**

Huandikwa kwa namna tofauti

- 7.4.15
- 7-4-2015
- 7/4/2015
- Julai 4, 2015

**Utangulizi**

Huwa mfupi na humlenga mwandikiwa

Mfano:

- Kwa mpendwa baba
- Kwa sahibu Jane

**Mwili/ kiwiliwili**

Huchukua lengo/ madhumuni ya mwandishi

Huanza kwa kutuma salamu- kujuliana hali

Mambo mengi huandikwa hapa

Lugha sanifu lazima itumike

Mwisho hutuma salamu kwa jamaa wengine au marafiki

**Wasalaam/ maagano**

Mwandishi humuaga mwandikiwa

Huonyesha uhusiano uliopo baina ya wawili hawa:

Mfano

- Ni mimi mwanao mpendwa
- Ni mimi babako
- Wako sahibu wa chanda na pete

**Tashbihi**

Tunapendana kama chanda na pete/ ulimi na mate/ kinu na mchi

Hutia bidii kama mchwa masomoni

Hutangamana kama mcwa masomoni

Hutangamana kama ulimi na mate

Mpole kama mwanakondoo

**Methali**

Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu

Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

Mtaka yote hukosa yote

Mvumilivu hula mbivu

Mtegemea nundu haachi kunona

**Muundo**

ANWANI

TAREHE

UTANGULIZI

MWILI/ KIWILIWILI

MAAGANO/ WASALAAM

**UMUHIMU WA MAJI**

Maji ni nini

Hupatikana wapi

**Manufaa**

Maji ni kiowevu kisicho na rangi, ladha au harufu

Maji hutokana na mvua

Mawingu hukusanyika na matone huanguka ardhini

Maji hupatikana mtoni, bwawani, maziwani, baharini na mashimoni

Hukusanyika baada ya mvua kunyesha

Chemichemi zina maji yabubujikayo kutoka ardhini na kufuata mkondo na huwa mto

Maji yana matumizi mengi mno

Ni makao ya wanyama- vyura, viboko, ngwena, samaki nk

**Nyumbani**

Hutumika kwa shughuli ainati kama vile:

Kuogea ili kutoa uchafu(nongo)

Kufulia lebasi/ nguo chafu

Kwa upishi

Kunwewa ili kukonga roho

Kuoshea vyombo

Kupigia deki sakafu na kupangusia nadirisha

**Kondeni/ shambani/ mgundani**

Kuchanganya kemikali ili kuua wadudu waharibifu

Kunyunyizia mimea-kiangazi

Kuoshea vifaa baada ya kazi kv.torori, panga, majembe

Kuwanywesha mifugo

Kufugia/ kuhifadhi samaki

Usafi wa jumla

**Viwandani**

Kuoshea kahawa(matunda)

Kutengeneza vinywaji –pombe, soda, sharubati

Kupoza mashine

Kutengeneza karatasi

Kuoshea chupa ili kuziweka vinywaji tena

**Burudani**

Kupiga mbizi

Chemichemi za maji yabubujikayo

Mvuke- ziwa bogoria huvutia watalii

**Usafiri**

Kuvuka kwenda ng’ambo

Manowali, motoboti, ngalawa, mtubwi, meli, husafiria majini

**Ulinzi**

Wanajeshi wa majini-sabmarinitashbihi

**Tashbihi**

Mizigo mizito kama nanga

Nuka kama beberu/ kodonda

Chafu kama fungo

Chakula kitamu kama uki, asali, halua

**Methali**

Maji ni uhai

Maji hufuata mkondo

Maji ukiyavulia nguo yaoge

Maji hayapandi mlima

Chura akitupwa majini hafi

**MWALIMU WETU**

Jina

Jinsia

Umri

Jamaa/ familia/ nasaba- mume/ mke, wana

Somo afundishalo

Madarasa afundishayo

Kwa nini unampenda

Huwasaidia vipi

Dini

Konde/ magari/ jumba

Ni wa jinsia ya kike / kiume

Ana mke/ mume mmoja

Mkewe ni mrembo kama mbega

Mumewe ni mtanashati na nadhifu

Ana wana wawili wafananao kama shilingi kwa ya pili

Ana umbo la duara

Urefu wa wastani-si mrefu si mfupi

Ngozi yake ni ya maji ya kunde, ni mweusi tititi makaa kando

Ana mwanya kwa meno yake ya mbele

Ana nywele ndefu nyeusi tititi

Hudira nywele zake na kukata kucha

Ana umri wa makamo/ takribani miaka arubaini

Huwa nadhifu na safi

Nguo zake hupigwa pasi na kunyooka twaa kama maiti

Huvalia vizuri, suti, rinda, tai, sketi, viatu

Hujipamba akapambika vizuri

Yeye hufundisha somo la Kiswahili na sayansi

Madarasa ya nne, tano na saba

Ana roho safi, nia nzuri na mikono wazi

Hutupa zawadi tukifaulu

Hututambia hadithi/ ngano tamutamu

Hutufunza vizuri, hutushauri kama mzazi

Ni mfuasi wa dini la kiislamu, kikristo

Ana jumba zuri na kuonewa fahari, magari mawili na konde la miwa

**Tashbihi**

Nyooka twaa! Kama mauti

Cheka kama radi

Pendeza kama hurulaini

**Methali**

Ukiona vyaelea jua vimeundwa

Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu

Wema hauozi

Baada ya dhiki faraja

**MNYAMA NIMPENDAYE**

Ni mnyama gani

Kama:Ngombe, njiwa, kuku, farasi, mbwa, bata, kanga

Jina la mnyama

Kama:Chausiku, mrembo, maria, mweusi, maridadi

Umbo

Mfano- mkubwa, mnene, mfupi

Rangi

Mfano-mweusi, mweupe, madoadoa, kijivu

Umri

Mfano-miaka miwili, mmoja, mitano, miezi mine, sita

Ulimpata wapi?

- Nilipewa zawadi na rais-kughani shairi baba/ babu/ bibi, mjomba,mama
- Nilimwokota njiani akiwa mchanga
- Nilimnunua

Faida zake

**Ng'ombe:**

- Hutupa maziwa
- Hutupa samadi
- Huzaa ndama-fahali wanachinjwa
- Ngozi, nyama, kwato, pembe
- Wanauzwa-fedha

**Kuku:**

- Samadi
- Mayai
- Manyoya
- Vifaranga

**Kanga**

- Pambo-kuvutia watu
- Samadi
- Mayai
- Manyoya

Hucheza naye wakati wa mapumziko

**Vyakula vyake**

- Nafaka
- Nyasi/ majani/ mimea
- Maji safi

**Makao yake**

- Zizi/ boma/ zeriba
- Kizimba
- Kibanda

**Humtunza vipi**

Kusafisha makao yake

Kumpulizia dawa kuwaua wadudu

Kumpeleka kwa daktari wa mifugo akiugua

Ng’ombe huogeshwa kwenye josho

Kumnywesha dawa kuangamiza wadudu hatari kama minyoo

Kumpa lishe bora

Kufanya mazoezi pamoja

**Tamati**

Tuwatunze wanyama kwa hali na mali

Wanyama wana faida telele kwa wanadamu

Ukiwa na wanyama na uwatunze utawa tajiri mtajika

**MUHULA WA PILI**

**LUGHA**

**SURA YA PILI**

**Ufahamu: mzee Mumunye (1)**

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu: mwalimu pamoja na wanafunzi-adodoe fani, mwanafunzi mmojammoja kimyakimya

Tathmini: mufti uk 113

Sarufi: Kiambishi ji

Kiambishi ni

Kueleza maana na matumizi ya kiambishi JI

**Mfano**

| Kati | mwisho |
|---|---|
| Mzee amejipikia | msomaji |
| Ninajiona | wakimbiaji |

Tathmini: mufti uk 116

Kurunzi uk 77

Kkd uk 32

**Kusikiliza na kuongea**

**Mafumbo**

Fumbo ni swali la chemshabongo linalohitaji utumizi wa akili kupata jibu

Mfano

Wazazi wawili waliagiza soda chupa tatu. Kila mmoja alinywa soda bila kugawa.je iliwezekanaje?

Tathmini: mufti uk 116

Kurunzi uk 140

**Kuandika: sentensi**

Kuwaongoza kuendeleza maneno na kuundasentensi

Kuwaongoza kuandikasenetnsi kwa herufi ndogo

Kuandika kwa herufi kubwa

Mfano

Matone ya mvua yalindondoka ndo ndo ndo

Tathmini: mufti uk 117

Kkd uk 191

**Msamiati: majina yam mea**

Mmea hutokana na mbegu

Huwa na matawi, mizizi na shina

Hupaliliwa ili istawi

**Mifano**

- Mahindi
- Maharagwe
- Mkunde
- Mtama
- Mgomba
- Mnyanya

Tathmini: mufti uk 122

Kurunzi uk 156

**SURA YA TATU**

**Ufahamu: mzee Mumunye (2)**

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana ya msamiati

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu: mwalimu pamoja na wanafunzi-adodoe fani, mwanafunzi mmojammoja kimyakimya

Tathmini: mufti uk 122

**Sarufi: kimilikishi –ANGU na –ETU**

Kimilikishi ni neon linaloonyesha nomino inamilikiwa na nani

Mifano

- Kikombe changu
- Mkate wangu
- Vikombe vyetu
- Vyandarua vyetu
- Mkeka wetu
- Mawe yetu

Tathmini: mufti uk 125

Kurunzi uk 87

**Kusikiliza na kuongea: mashairi**

Shaairi ni wimbo wa Kiswahili

Hutungwa na malenga na kughaniwa na manji

Kweleza msamiati

Mfano

Mshororo, ubeti, manju, malenga

Tathmini: Kurunzi uk 90

**Kuandika: kinyume**

Kinyume ni tofauti iliyopo baina ya vitu viwili

Mfano

- Mnene mwembamba
- Mgeni mwenyeji
- Konda nenepa

Tathmini: mufti uk 126

**Msamiati: hospitalini**

Hospitali ni mahali pa kufanyiwa matibabu

Zahanati, kliniki, dispensary ni hospitali ndogo

Mfano

- Mwuguzi/nesi
- Daktari/ mganga
- Plasta
- Machela
- Dawa
- Sindano
- Bandeji
- Glovu
- Kipimajoto

Tathmini: mufti uk 129

Kurunzi uk 133

Kkd uk 224

**SURA YA NNE**

**Kusoma: ufahamu**

Mzee mumunye (3)

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu: mwalimu pamoja na wanafunzi-adodoe fani, mwanafunzi mmojammoja kimyakimya

Tathmini: mufti uk 133

**Sarufi: wakati HU**

Hutumika kuonyesha kitendo hutendeka kila siku au mara kwa mara

Mfano

- Mimi hula
- Hula matunda
- Yeye hupiga mswaki
- Husoma kwa bidii
- Humcha Mungu
- Hupiga mbizi

Tathmini: mufti uk 134

Kkd uk 112

**Kusikiliza na kuongea**

**Methali**

Methali ni fumbo fupi lenye maana fiche

Huelimisha, huonya, huburudisha

Mfano

- Haba na haba hujaza kibaba
- Panya wengi hawachimbi shimo
- Njia ya mwongo ni fupi
- Motto wa kuku hafunzwi kuchakura
- Akili ni mali

Tathmini: mufti uk 135

Kurunzi uk 109

Kkd uk 69

**Kuandika: imla**

Kuwaongoza na kuwasomea kifungu mara moja

Kuwasomea mara ya pili wakiandike

Kusoma kwa kufululiza

Kifungu- magonjwa ni maradhi

Tathmini: mufti uk 135

**Msamiati: akisami**

Akisami ni sehemu ya kitu kizima

Mfano

- Nusu
- Theluthi
- Robo
- Humsi
- Subui
- Sudusi
- Thumni
- Tusui
- Ushuri

Tathmini: mufti uk 137

Kurunzi uk 146

Kkd uk 150

Mazoezi ya ziada: kkd uk 211

**SURA YA TANO**

**Kusoma: ufahamu**

Sungura mwenye pembe

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu: mwalimu pamoja na wanafunzi-adodoe fani, mwanafunzi mmojammoja kimyakimya

Tathmini: mufti uk 141

**Sarufi: viunganishi**

Viunganishi ni maneno yanayounganisha maneno au sentensi kwa minajili ya kuleta maana

Mfano

- Kwa sabau
- Bila
- Wala
- Lakini
- Ila
- au

Tathmini: mufti uk 145

Kurunzi uk 105

Kkd uk 79

**Kusikiliza na kuongea**

**Mjadala**

Mjadala ni mazungumzo yanayohusu mada mahususi ili kujenga hoja

Shule za malazi ni bora kuliko za kutwa

| Malazi | kutwa |
| --- | --- |
| Muda wa kusoma ni mrefu | kuenda nyumbani kila siku |
| Si bora sana | vyakula bora |
| Bei ghali | bei rahisi |

Tathmini: Kurunzi uk 154

Kkd uk 130

**Kuandika**

**Mtiririko wa sentensi**

Sentensi huundwa kwa neon au maneno

Mfano

- Tutaenda nyumbani
- Mdogo alilala mtoni chini      motto mdogo alilala chini
- Vitabu nipe vyote      nipe vitabu vyote

Tathmini:      mufti uk 145

Kkd uk 16


**Msamiati**

**Pembe nne za dunia**

Kifaa cha kuonyesha pembe hizo huitwa dira

Pembe nne kuu ni kaskazini, kusini, mashariki

Magharibi




Tathmini:      mufti uk 146,158

Kurunzi uk 183

Kkd uk 156

Ziada: kkd uk 206

## SURA YA SITA

**Kusoma: ufahamu**

Mpanda ovyo huvuna ovyo

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu: mwalimu pamoja na wanafunzi-adodoe fani,

mwanafunzi mmojammoja asome kimyakimya

Tathmini: mufti uk 149

**Sarufi**

**Vihusishi**

Vihusishi ni maneno yanayoonyesha uhusiano baina ya watu vitu au wakati

Mfano

- Kabla ya
- Baada ya
- Kati ya
- Miongoni mwa
- Nyuma ya
- Nje ya
- Chini ya

Tathmini: mufti uk 153

Kkd uk 99

**Kusikiliza na kuongea**

**Shairi**

Shairi ni wimbo wa kiswahili

Malenga, manju, kughani, mshororo, ubeti, kibwagizo

Mada: usifu kwa wazazi

Tathmini: mufti uk 153

**Kuandika**

Hati: umoja na wingi

Hati ni mwandiko

Mifano

- Mama zetu walivinunua vikombe hivi
- Mama yangu alikinunua kikombe hiki
- Matunda haya mekundu ni yenu
- Tunda hili jekundu ni lako

Tathmini: mufti uk 155

Kurunzi uk 71

**Msamiati**

**Tarakimu (1,001- 5,000)**

Tarakimu ni nambari au rakamu

Tarakimu pia ni alama ya hesabu ya kuonyesha idadi

Mifano

1,001 elfu moja na moja

1,999 elfu moja mia kenda tisini na kenda

3,007 elfu tatu na saba

5,000 elfu tano

Tathmini: mufti uk 156

Kurunzi uk 159

## SURA YA SABA

**Kusoma**

**Ufahamu: motto mvivu na mvuvi**

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu: mwalimu pamoja na wanafunzi-adodoe fani,

mwanafunzi mmojammoja asome kimyakimya

Tathmini: mufti uk 158

**Sarufi**

**Viashiria hiki na hivi**

Kiashiria pia huitwa kionyeshi

Huonyesha/ huashiria ilipo nomino

Hiki na hivi hutumika pamoja na ngeli ya KI-VI kwa umoja na wingi

Mfano

- Kiatu hiki kimeraruka — viatu hivi vimeraruka
- Kitabu hiki kinapendeza — vitabu hivi vinapendeza
- Chandarua hiki kinakinavutia — vyandarua hivi vinavutia

Tathmini: mufti uk 160

Kkd uk 139

**Kusikiliza na kuongea**

**Mawasiliano**

Kuwasiliana ni kupashana habari

Mifano

- Simu
- Magazeti
- Video
- Rununu
- Majarida
- Tarakilishi
- Runinga
- Barua
- Satalaiti
- Faksi
- Tondomiza
- Kipepesi

Tathmini: Kkd uk 146

**Kuandika**

**Nomino kutokana na vitenzi**

Nomino ni jina la kitu, mtu au hali

Kitenzi huonyesha kitendo

Kuwaongoza kuigiza baadhi ya vitenzi

Kutaja watendaji –nomino

Mfano

- Funza mfundishaji
- Chora mchoraji
- Hama mhamaji
- Choma mchomaji
- Vuna mvunaji

Tathmini: mufti uk 161

**Msamiati**

**Tarakimu(5,000-10,000)**

Tarakimu ni idadi ya nambari

Tarakimu pia huitwa rakamu au nam,bari

Mifano

5,015 elfu tano na kumi na tano

7,707 elfu saba mia saba na saba

8, 508 elfu nane mia tano na nane

9,696 elfu tisa mia sita tisini na sita

Tathmini: mufti uk 162

Kurunzi uk 199(ziada)

**SURA YA NANE**

**Kusoma**

**Ufahamu: jogoo aliyemshinda samba**

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu:

a. mwalimu pamoja na wanafunzi-adodoe fani,
b. mwanafunzi mmojammoja asome
c. wanafunzi wasome kwa kiada

Tathmini: mufti uk 166

**Kusikiliza na kuongea**

**Viashiria hili na haya**

Kiashiria pia ni kionyeshi

Huonyesha ilipo nomino inayorejelewa

Hili na haya hutumika pamoja na ngeli ya LI-YA

Mfano

| | |
|---|---|
| Jembe hili | majembe haya |
| Ua hili | maua haya |
| Shati hili | mashati haya |
| Godoro hili | magodoro haya |

Tathmini: mufti uk 169

Kkd uk 106

**Kusikiliza na kuongea**

**Hadithi**

Hadithi pia huitwa ngano au hekaya

Ni masimulizi ya visa au matukio

Utangulizi:

Paukwa pakawa

Hadithi hadithi

Tathmini: wanafunzi wasimulie hadithi

**Kuandika**

**Hati: kifungu**

Kifungu ni kikundi cha sentensi

Hupangwa katika aya

Mfano

Mbu ni hatari

Wanafunzi waelekezwe kuandika kwa hati nadhifu

Tathmini: mufti uk 169

**Msamiati**

**Mavazi**

Mavazi ni nguo au viatu vivaliwavyo kwa sehemu tofauti

Husetiri uchi, huzuia hali mbaya za anga na pia hurembesha

Mifano

- Gagro/ gagulo
- Kikoi
- Kabuti
- Kizibao
- Kanchiri/ sindiria
- Shimizi/ kamisi
- Patipati
- Chepeo

Tathmini: mufti uk 170

Kkd uk 162

Kurunzi uk 149

## SURA YA TISA

**KUSOMA**

**Ufahamu: usafiri wa matwana**

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu:

a. mwalimu pamoja na wanafunzi-adodoe fani,
b. mwanafunzi mmojammoja asome
c. wanafunzi wasome kwa kiada

Tathmini: mufti uk 176

**Sarufi**

**Vivumishi vya sifa**

Kivumishi ni neon linaloeleza nomino

Kivumishi cha sifa huonyesha na kueleza sifa, hali au jinsi nomino ilivyo

Mfano

Ngeli

| | |
|---|---|
| A-WA | Motto mkubwa |
| | Watoto wakubwa |
| KI-VI | Kiatu kikubwa |
| | Viatu vikubwa |
| LI-YA | Jani kubwa |
| | Majani makubwa |

Tathmini: mufti uk 177

Kurunzi uk 151

**Kusikiliza na kuongea**

**Vitendawili**

Kitendawili ni swali la chemshabongo linalotatiza kupata jibu

Huwa na mianzo maalum

Kitendawili!

Tega

Mfano:

- Mtoto wangu nikimwogesha hakauki
- Mvua inanyesha mlima unapanda
- Nikimwogesha mwanangu anaconda
- Bingiri! bingiri! Twende Butere
- Kenua kenua tupate mvua

Tathmini: mufti uk 178

Kkd uk 29

Kurunzi uk 69

**Kuandika**

**Imla: shambani**

Kuwaongoza kutaja baadhi ya msamiati

Kuwapa imla

Mfano

- Kupalilia
- Kupogoa
- Kunawiri
- Kunyunyizia
- Rutuba
- Kupanda
- Kuatika
- Kuvuna
- Mche
- Mashina
- Kustawi
- Kufyeka

Tathmini: kurunzi uk 15

**Msamiati**

**Viumbe na makazi yao**

Makazi ni makao au mahali pa kuishi

Viumbe ni wanyama ambao wana uhai

Mifano

- Nyuni kiota
- Ng’ombe zizi / zeriba / boma
- Nyuki mzinga
- Samaki majini
- Konokono kombe

Tathmini: mufti uk 181

Kurunzi uk 205 (ziada)

## MUHULA WA PILI INSHA

### NYUMBANI KWETU

Vidokezo

Maana ya nyumba

Aina ya nyumba

- Msonge
- Mawe
- Ya udongo
- Ghorofa

Umbo la nyumba yetu

Nyumba inapatikana wapi

Sehemu za nyumba yetu

**Sebule na vifaa vinavyopatikana pale**

- Redio
- Runinga
- Zulia
- Meza
- Kabati
- Mapazia
- Busati
- Rafu
- Redio
- Kinanda
- Friji/ jokofu

**Jikoni**

Mahali pa kupikia vyakula

Vifaa vinavyopatikana hapa ni

- Vyungu
- Birika
- Chano
- Karo
- Seredani
- Kinu na mchi
- Sufuria
- Vikombe
- Jiko la gesi/ umeme
- Buli
- Sinia
- Takia
- Sahani

**Vyumba vya malazi**

Ni vingapi

Vifaa ni kama

- Vitanda
- Blanketi
- Magodoro
- Mto
- Foronya
- Shubaka
- Masaduku

Bafuni/ hamamuni

- Sabuni
- Taulo
- Sifungo
- Bilula za maji
- Dodoki

**Msalani**

- Karatasi shashi
- Haja ndogo
- Haja kubwa

**Mazingira nje ya nyumba**

- Bustani la maua yanayopendeza kama hurulaini wa peponi
- Maegesho
- Miti yenye kivuli
- Kidibwi cha kuogelea

**Methali**

- Mwacha mila ni mtumwa
- Chema chajiuza, kibaya chajitembeza
- Heshima si utumwa

**Tashbihi**

- Ng'ara kama mwezi
- Tamu kama halua/ asali
- Maridadi kama mbega
- Nyeupe kama theluji
- Metameta kama nyota angani

**Misemo**

- Piga koga
- Piga mswaki
- Shtaki njaa
- Andika meza
- Tia nakshi
- Piga mbizi

**Tanakali za sauti**

- Lala fofofo
- Bonyea bonye bonye

**Miundo ya sentensi**

Nimezaliwa nikalelewa na kuishi huko kwa miaka na mikaka

Dirishani pamefunikwa kwa mapazia ya Hariri

Jikoni ndipo vyakula na mapochopocho matamu kama halua huandaliwa

Ndani ya jokofu mna sharubati ya karakara, zabibu na maziwa gururu

Sebuleni utaliona zulia linalometameta na kung’aa waa kama mwezi

Siwezi kudharau kwetu, chambilecho waswahili, mwacha mila ni mtumwa

Vitanda vimetandikwa vikatandikwa

**NG’OMBE WETU**

Ng’ombe ni mnyama gani na maumbile yapi

- Maana ya ng’ombe
- Ana miguu mingapi
- Ana pembe ngapi

Jina la ng’ombe wetu

- Ulimpataje ng’ombe huyu
- Ulinunua ama ulipewa kama zawadi
- Mbona ukampa jina hilo

Tabia za ng’ombe wetu

- Ni mpole ama ni mkali
- Akiwa mpole hufanya nini
- Je, yeye hupenda kuishi na wengine?

Huishi wapi

- Boma/ zizi/ zeriba
- Umemjengea zizi

Yeye hula nini

- Je, wewe humletea nyasi akiwa zizini
- Yeye hula mboga na majani
- Ushamnunulia chakula cha dukani

Manufaa ya ng’ombe wetu

- Kutupatia mbolea
- Kuwazaa ndama
- Kutupatia maziwa

Jinsi ninavyomtunza

- Kumlisha vizuri
- Kuhakikisha hanyeshewi wala kuchomwa sana na jua
- Kutibiwa mara kwa mara na daktari wa mifugo

**Msamiati**

Ng’ombe ni mfugo

Hufugwa nyumbani na wakulima

Hukamwa maziwa ndoo mzima

Humpeleka malishoni au machungani

Kinyesi chake hutumiwa kama mbolea

**Tashbihi**

Eupe kama theluji

Mweusi kama makaa

Mnene kama nguruwe

Tamu kama halua

Mpole kama mwanakondoo

Mkali kama samba

**Maneno magumu**

- Samadi
- Fuga
- Mbolea
- Ndama
- Zeriba/ zizi/ boma
- Hayawani
- Kiamboni

**Muundo wa sentensi**

Ng’ombe ni hayawani anayefugwa kiamboni na binadamu

Yeye hula nyasi na nyakati nyingine humnunulia vyakula vya dukani

Ng’ombe wetu huzaa ndama kila baada ya miaka miwili

Samadi yake hutumiwa kama mbolea ili kuongeza rutuba kwenye mchanga

Ng’ombe wetu anapougua, mimi humwita daktari wa mifugo ili kumtibu

**UMUHIMU WA MAJI**

Maana ya maji

Kiowevu kinachopatikana kwenye mito, maziwa, baharini KINACHOTOKANA NA MVUA

Maji yana faida telele/ sufufu/ tolatola/chungu nzima kwa binadamu, wanyama na mimea

Baadhi ya faida/ manufaa ya maji ni:

Hutumiwa kwa upishi wa vyakula na vinywaji ainati

Hutumiwa kwa usafiri hasa vyombo vya majini kama:

- Motoboti

- Mashua
- Ngalawa
- Nyambizi
- Merikebu

Hutumiwa kwa usafi wa mwili, mazingira na mavazi

Huuzima moto unapoteketeza vitu

Ni makao ya samaki na wanyama wengine kama mamba, viboko, nyangumi

Hutumika katika michezo na kuburudisha kv. Kuogelea-kupiga mbizi

Hutumiwa kukata kiu

Hutumiwa kunyunyizia mimea wakati wa kiangazi/ ukame

Huzungusha mashine na mitambo ili kutoa nguvu za umeme

Kupoza injini zim\napokuwa moto

**Msamiati**

Nishati au nguvu za umeme

Maradhi tumbitumbi kama kipindupindu, homa ya matumbo

Huimarisha siha/ afya

Shehena ya mizigo

Mchafu kama fuko

Kwenda jongomeo

Kustawi na kunawiri

Hamamu na madibwi

**Methali**

Maji hufuata mkondo

Mkamia maji hayanywi

Atanguliaye kisimani hunywa maji maenge

Mfa maji haachi kutapatapa

**Muundo wa sentensi**

Maji yana matumizi kochokocho kwa binadamu , mimea na wanyama

Maji huzuia maradhi tumbitumbi yanayoweza kuwasafirisha watu hadi jongomeo

Mimea inaponyunyiziwa maji hunawiri na kustawi vyema

Baadhi ya watu hupiga mbizi kwenye madibwi ya maji

Maji ya baharini hutumika kusafirisha shehena na mizigo miziti kama nanga

**MIMI**

Jina langu ni nani, jinsia

Unaishi wapi

Wazazi wako ni nani, kazi zao

Ndugu zako ni nani

Umri wa miaka mingapi

Umbo lako

- Mnene tipwa tipwa kama nguruwe
- Mrefu kama unju/ mlingoti
- Mfupi kama nyundo
- Mwembamba kama ng'onda
- Mweusi kama makaa/ lami/ mpingo

Unasomea shule gani

- Darasa gani
- Somo ulipendalo
- Mwalimu umpendaye

Marafiki wako ni nani

- Wanaishi wapi
- Wanasomea wapi

Chakula na kinywaji upendacho

Mavazi upendayo

Mchezo uupendao

- Kandanda
- Kwata
- Jugwe
- Voliboli
- Riadha

Unapenda kutazama nini

Ungetaka kuwa nani siku za usoni

Hitimisho

**Tashbihi**

- Bidii kama mchwa
- Mweupe kama mzungu
- Mcheshi kama kibonzo
- Pendana kama chanda na pete
- Maridadi kama mbega
- Mrembo kama upinde wa mvua
- Tamu kama asali/ halua/ uki

**Tanakali za sauti**

- Nyooka twaa!
- Mweupe pep e pe!
- Mweusi tititi!
- Mrefu njorinjori!
- Tulia tuli!

**Methali**

- Heshima si utumwa
- Mvumilivu hula mbivu
- Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki
- Mtaka cha mvunguni sharti ainame
- Haba na haba hujaza kibaba

**Muundo wa sentensi**

Mimi ni mvuli/ ghulamu/ mvulana

Mimi ni:

Mwanabee/ kifungua mimba

Kitindamimba/ kifungamimba/ mziwada

Naishi mjini Nairobi katika mtaa wa Huruma karibu na kiwanda cha chumvi

Mimi ni mwanafunzi mwenye adabu na heshima kwa wakubwa chambilecho wahenga heshima si utumwa

Nina kimo cha wastani. Mimi si mrefu kama mlingoti wala mfupi kama nyundo

Rafiki yangu ni mcheshi kama kibonzo

**Msamiati**

Mziwada/ mwanabee

Mcheshi

Mvuli/ ghulamu/ mvulana

Banati/ msichana

Wavyele/ wazazi

Sahibu/ mwandani/ rafiki

Kitongoji/ kijiji

Kiamboni/ nyumbani

Umri/ hirimu

Runinga / televisheni

Kandanda/ soka/ kabumbu

Furaha ghaya

Hamu na ghamu

**BARUA YA KIRAFIKI**

Barua hii pia huitwa barua ya kidugu

Barua pia huitwa waraka

Barua hii huwa ya kuwasiliana na kujuliana hali

Barua hii huhusu watu wenye uhusiano Fulani:

Familia/ ukoo / nasaba/ aila

Marafiki/ wandani/ sosmo/ masahibu/ mwenza

Mambo muhimu ya kuzingatia

**Anwani:**

Huandikwa kulia pembeni

Anwani hii moja huwa ya mwandishi

Sanduku la posta

Mahali ilitoka

Mfano

Shule ya msingi ya Lizar

S.L .P 1910

NAIVASHA

**Tarehe:**

Huonyesha siku ambayo barua hii iliandikwa

Mfano

- Aprili 10 ,2015
- 10/10/2015
- 10-4-2015

**Kianzio**

Hutiwa kushoto karibu na pambizo

Hutumia herufi ndogo

Hutumia koma mwishoni

Mfano

- Kwa rafiki mpendwa Zainabu,
- Kwa somo wangu wa chanda na pete Bahati’

**Utangulizi**

Huhusu kumjalia mwenzio hali-maamkuzi

Mfano

- Hujambo?
- Natumai u buheri wa afya
- Familia yako iko vipi?
- Pokea salamu chekwachekwa/ sufufu
- Natumai u mzima kama kigongo
- Pokea salamu fokofoko kama mchanga baharini

**Mwili/kiwiliwili**

Sehemu hii ndiyo uti wa insha

Mtahiniwa anatarajiwa kulenga swali la mtahini

Mfano

- Mwandikie rafiki yako barua ukimweleza jinsi unavyoendelea na masomo
- Mtahiniwa aandike jinsi anavyoendelea shuleni

Mfano

- Ninafanya bidii za mchwa za kujenga kichuguu
- Ninabingirisha gurudumu la masomo
- Tunashirikiana na wenzangu kama jembe na mpini/ kinu na mchi/ kiko na digali
- Ninauliza maswali kwani kuuliza si ujinga

**Hitimisho**

Kumwaga mwenzako na kumtakia heri njema

Mfano

- Wasalimu wazazi, ndugu, marafiki
- Tutazidi kuongea kwani barua ni nusu ya kuonana
- Kalamu yangu inalia wino
- Ninakunja jamvi
- Nimefika tamati
- Mungu akubariki
- Mola awaneemeshe Baraka za kozole/ sufufu

Kuhitimisha kwa jina la mwandishi

Mfano

- Wako wa chanda na pete

  Kalfan Juma

- Ni mimi wako wa mate na ulimi

  Bahati Nasibu

Sampuli

Shule ya msingi ya lizar,

S.L.P 1910,

NAIVASHA.

APRILI 9,2015

Kwa rafiki mpendwa BAHATI NASIBU,

Utangulizi

Mwili

Ni mimi wa chanda na pete,

Kalfan Juma.

**Tashbihi**

Safi kama mfuaji

Bidii za mcwa

Bidii za duduvule

Taratibu kama jongoo

Rahisi kama kula papai kwa kijiko

**Misemo**

Jifunga nira

Kujikaza kisabuni

**Methali**

Barua ni nusu ya kuonana

Kuuliza si ujinga

Elimu ni bahari

**JINSI NILIVYOSHEREHEKEA SIKUKUU YA KRISMASI**

Vidokezo

Kuamka na kujitayarisha

- Kuoga na kupiga mswaki
- Kuvalia mavazi nadhifu

Kunywa staftahi na kuaga jamaa

Kupitia kwa sahibu kumwita

- Kuwasili kwao
- Kupata amejiandaa

Kuelekea kanisani

- Safari
- Wingi wa watu

- Kuwasili kanisani

Kufanyika kwa ibada

- Injiri/ bibilia takatifu
- Nyimbo kuimbwa
- Sadaka kutolewa/ zaka

Kuelekea kwenye bustani kujistarehesha

- Kubembea/ kupiga gumzo
- Kupigwa picha
- Kuendesha farasi

Kuelekea nyumbani

- Msongamano wa watu na magari
- Kuagana na rafiki
- Kuwasili nyumbani.saa ngapi

Maakuli mazuri

- Aina mbalimbali za matunda-matufaha, mananasi
- Aina mbalimbali za vinywaji-karakara, soda
- Aina mbalimbali za vyakula-pilau, nyama

Kula hadi kushiba

Kuenda kulala

- Usingizi wa pono
- Ndoto njema

**Tashbihi**

- Tamu kama halua
- Sauti nyororo kama ninga
- Haraka kama umeme
- Ngara kama mbalamwezi
- Ringa kama tausi
- Majina ya makundi
- Umati wa watu
- Halaiki ya watu
- Mlolongo wa magari

- Safu ya milima

**Misemo**

- Kungoa nanga
- Kupiga mbweu
- Kupiga milundi
- Piga mswaki

**Methali**

- Polepole ndio mwendo
- Mwenye macho haambiwi tazama
- Haraka haraka haina Baraka

**Muundo wa sentensi**

Rafiki yangu alikuwa amengara kama mbalamwezi

Watu waliimba nyim,bo kwa furaha mithili ya tasa aliyejikopoa pacha salama salmini

Nilijitayarisha polepole  kwani nilielewa maana ya methali, polepole ndiyo mwendo

Niliingiwa na furaha na buraha baada ya kumwona rafiki yangu

Nilivaa mavazi nadhifuyaliyopigwa pasi yakanyooka twaa

Tulikula mapochopocho ainati yaliyokuwa matamu kama asali ya malkia nyuki

**AJALI BARABARANI**

Ajali ni tukio lenye madhara linalotokea ghafla

Husababisha maafa au majeraha

Mwanafunzi anahitajika kusimulia kisa kinachohusisha magari, baiskeri au pikipiki katika ajali

Katika insha hii mtahiniwa azingatie vipengele hivi:

Ulikuwa wakati gani ajali ilipotokea

Alikuwa akielekea wapi aidha kwa garia au kwa miguu

Ajali yenyewe ilihusisha nini

Ni nini kilichofuatia baada ya ajali hiyo: hisia za wahusika’ kuagiza msaada kwa majirani au polisi

**Msamiati**

Kuamka jogoo la kwanza

Demka/ rauka majogoo

Piga mswaki

Koga hamamuni kwa dodoki/ sifonga

Kujikwatua kwatukwatu/ kujipamba pambepambe

Valia libasi zilizongaa kama mbalamwezi

Gari kutiwa moto na dereva/ mshika usukani

Kungoa nanga

Klaa karibu na dirisha kujionea mandhari yaliyovutia

Kujifunga mkanda wa usalama

Piga soga/ gumzo/ porojo

Mwendo wa kasi kama duma/ risasi/ umeme

Gurafu

Matuta

Yumbayumba

Shindwa kudhibiti gari

Gongana dafrau/ ana kwa ana

Bingirika bingiribingiri

Vigae vigae

Damu kutiririka tiriri

Vilio vilienea kote

Machozi ya majonzi

Machozi yalipukurika puku puku

Ving'ora vya ambulensi na makaradinga

Huduma ya kwanza

Kuwanusuru manusura

Kulilia uhai wao

Kupelekwa:

- Thieta
- Wodi
- Sadaruki kwa majeruhi

Kufungwa

- Plasta
- Kitata
- Bendeji

Wafu kupelekwa mochari/ ufuoni/ makafani

Tembe

Kifo kichungu

Kushika tama/ kumaka/ duwaa/ bung'aa

Mkasa huo utasalia katika kumbukumbu zangu

Nusurika katika tundu la sindano

Ponea chupuchupu

**Tanbihi:**

Mwanafunzi aeleze kuhusu funzo alilopata

**Methali**

Ajali haina kinga

Ajali haijali

Polepole ndio mwendo

Mwenda pole hajikwai

Haraka haraka haina Baraka

Mbio za sakafuni huishia ukingoni

**MUHULA WA TATU**

**LUGHA**

**Sura ya kwanza**

**Ufahamu: mkuu wangu (1)**

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu:

a. mwalimu pamoja na wanafunzi-adodoe fani,
b. mwanafunzi mmojammoja asome
c. wanafunzi wasome kwa kiada

Tathmini: mufti uk 189

**Sarufi**

**Vivumishi vyasifa – TAMU**

Kivumishi ni neon linalotoa maelezo zaidi kuhusu nomino

Kivumishi cha sifa hueleza jinsi nomino inaonekana au inavyofikiriwa

Sifa: tamu huonyesha ladha inayovutia

Mifano

| | |
|---|---|
| Chakula kitamu | vyakula vitamu |
| Mkate mtamu | mikate mitamu |
| Maneno matamu | neon tamu |
| Tunda tamu | matunda matamu |

Tathmini: mufti uk 192

Kkd uk 155

**Kusikiliza na kuongea**

**Mafumbo**

Fumbo ni swali lka chemshabongo linalomhitajimtu kukuna kichwa kupata jawabu mwafaka

Mfano

- Nina nyama yangu. Mkia si mtamu,kiwiliwili ni kitamu, kichwa ni kitamu zaidi
- Nne amekalia nne akingoja nne

Tathmini: mufti uk 192

Kurunzi uk 140

Kkd uk 83

**Kuandika**

**Kuendeleza maneno**

Kuwaelekeza kuandika maneno vizuri

Mfano

- Pelo pole
- Tenasa asante
- Kashimoo shikamoo

Kutunga sentensi kwa hayo maneno

Mfano

- Nilimwambia mama asante
- Pole kwa uchovu
- Naomba unipe kalamu

Tathmini: mufti uk 193

**Msamiati**

**Maumbo**

Umbo ni mchoro unaoonyesha kitu kilivyo au kinavyoonekana

Mifano

- ❖ Pia
- ❖ Tao
- ❖ Duara dufu
- ❖ Mstatili
- ❖ Pembe tatu
- ❖ Zigizagi
- ❖ Mraba
- ❖ Mistari sambamba
- ❖ Mche mraba
- ❖ Mche mstatili
- ❖ Mche duara
- ❖ Hilali
- ❖ Kopa
- ❖ Wimbi
- ❖ Mraba
- ❖ Shupaza
- ❖ Pau
- ❖ Uru
- ❖ Piramidi
- ❖ Hori

Tathmini: mufti uk 29

Kurunzi uk 25,111

Kkd uk 219

**SURA YA PILI**

**Kusoma**

Ufahamu: Mkuki wangu (2)

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu:

a. mwalimu pamoja na wanafunzi-adodoe fani,
b. mwanafunzi mmojammoja asome
c. wanafunzi wasome kwa kiada

Tathmini: mufti uk 195

Sarufi

**Vivumishi vya sifa –PYA**

Kivumishi cha sifa hueleza jinsi nomino ilivyo mfano: rangi, hisia, kimo

Mfano

Ngeli mfano

| | |
|---|---|
| A | Motto mpya ametumwa |
| WA | Watoto wapya wametumwa |
| KI | Chandarua kipya kimeletwa |
| VI | Vyandarua vipya vimeletwa |
| LI | Jiko jipya linavutia |
| YA | Majiko mapya yanavutia |

Tathmini: mufti uk 199

Kurunzi uk 150

**Kusikiliza na kuongea**

**Maigizo: ulevi**

Kulewa ni kupotewa na fahamu baada ya kuingilia uraibu wa ulevi

Wanafunzi wagawanyike katika vikundi

Wapewe mwelekeo wa kuigiza

Tathmini: wanafunzi washiriki maigizo

**Kuandika**

**Tarakimu 1,001-10,000**

Tarakimu ni idadi ya rakamu za nomino

Mifano

Wanajeshi 9,209 elfu tisa mia mbili na tisa

Siku 1,002 elfu moja na mbili

Samaki 4,503 elfu nne, mia tano na watatu

Tathmini: mufti uk 251

**SURA YA TATU**

**Kusoma**

Ufahamu: mkuki wangu (3)

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu:

a. mwalimu pamoja na wanafunzi-adodoe fani,
b. mwanafunzi mmojammoja asome
c. wanafunzi wasome kwa kiada

Tathmini: mufti uk 204

**Sarufi**

**Sifa –CHAFU**

Kivumishi cha sifa hueleza jinsi nomino ilivyo kv. Chafu, safi,

Chafu huchukua viambishi ngeli

Mifano

- Tunda chafu haliliwi
- Nguo chafu haivaliwi
- Maji machafu huleta maradhi
- Mikate michafu haitaliwa na wageni
- Ugali mchafu si mzuri kwa mili yetu

Tathmini: mufti uk 206

Kurunzi uk 150

**Kusikiliza na kuongea**

**Kuigiza haki za watoto**

Kuigiza na kuchukua nafasi ya nomino na kutenda kama nomino

Kuchambua picha

Kujadili haki za watoto

Kuteua wanafunzi wasome na kuigiza katika vikundi

Haki za watoto

- Kupewa elimu
- Lishe bora
- Kutengwa na tamaduni zisizofaa
- Kupewa malezi mema

Tathmini: wanafunzi waigize

**Kuandika**

**Kuendeleza maneno**

Kuendeleza ni kuandika kwa mfululizo

Kuwaongoza kuendeleza

Mifano

- Arthi ardhi
- Chaguwa chagua
- Chukuwa chukua
- Kitofu kitovu
- Huzuni mwingi huzuni nyingi
- Asubui asubuhi
- Bembelesa bembeleza
- Kukaranga kukaanga

Tathmini: mufti uk 208

**Msamiati**

**Viungo mwili: sehemu za ndani za mwili**

Hizi ni sehemu zinazopatikana kichwani na ndani ya mwili

Hazionekani wazi na eksrei lazima iwe

Mifano

- Ubongo
- Moyo
- Meno
- Ini
- Mapafu
- Ulimi
- Ufizi
- Moyo
- Koromeo
- Utumbo mchanga mwembamba
- Mifupa
- Mbavu
- Mishipa

Tathmini: mufti uk 209

Kurunzi uk 102, 107

Kkd uk 97(ziada)

**SURA YA NNE**

**Kusoma**

**Ufahamu: hadithi**

Hadithi ni masimulizi yanayoeleza matukio katika kisa

Pia huitwa ngano au hekeya

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu

Mwalimu pamoja na wanafunzi wakichambua fani za lugha zilizotumika

Mwanafunzi mmoja mmoja kwa kupokezana

Mwanafunzi asome kwa kiada

Tathmini: wanafunzi wasimulie hadithi kwa zamu

**Sarufi**

**Sifa- EMA**

Sifa EMA ni kivumishi kinachoelezea ubora wa nomino husika

Mfano

- Motto mwema
- Uji mwema
- Jani jema
- Ugali mwema
- Chandarua chema
- Swali jema
- Maji mema
- Nyumba njema
- Undu mwema
- Kandawala mwema

Tathmini: mufti uk 213

Kurunzi uk 150

**Kusikiliza na kuongea**

**Adabu na heshima**

Kuwa na adabu na heshima ni kutenda yanayokubaliwa na jamii na watu

mfano

- Tafadhari
- Asante
- Simile
- Pole
- Naomba
- Samahani
- Karibu
- Niwie radhi
- Sentensi
- Naomba kwenda haja
- Pole kwa uchovu
- Makiwa kwa kuachwa na ndugu
- Karibu kwetu

Tathmini: mufti uk 214

Kurunzi uk 13

**Kuandika**

**Sentensi :wingi**

Wingi ni jumla ya zaidi ya moja

Mfano

- Mchango ulitolewa
- Michango ilitolewa
- Mwezi utaisha
- Miezi itaisha
- Mswaki umezeeka
- Miswaki imezeeka

Tathmini: Kurunzi uk 18

**Msamiati**

**Marudio ya msamiati mbalimbali**

Mfano

- Ugonjwa
- Shuleni
- Nyakati
- Rangi
- Ukoo
- Nyuni
- Sehemu za mwili za nje
- Watu na kazi zao

Tathmini: mufti uk 215,216

Kkd uk 106

**SURA YA TANO**

**Kusoma:**

Ufahamu: ufagio wa maji

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu:

a. mwalimu pamoja na wanafunzi akieleza fani za lugha
b. mwanafunzi wasome kwa kupokezana mmojammoja
c. wanafunzi wasome kwa kiada

Tathmini: mufti uk 219

**Sarufi**

**Sifa-Bovu**

Sifa –BOVU ni kuvumishi cha sifa kinachoonyesha jinsi nomino ilivyo kwa ubora

Bovu huonyesha imeharibika

Mfano

| | |
|---|---|
| Tunda bovu | Matunda mabovu |
| Jani bovu | Majani mabovu |
| Uzi mbovu | Nyuzi bovu |
| Chakula kibovu | Vyakula vibovu |
| Tabia mbovu | Tabia mbovu |
| Maziwa mabovu | maziwa mabovu |

Tanbihi: ngeli ya LI-YA majina hayachukui kiambishi katika umoja

Tathmini: mufti uk 221

Kkd uk 150

**Kusikiliza na kuongea**

**Vitendawili**

Kitendawili ni viteguzi vinavyotegwana majibu hayapatikani waziwazi

Mwanzo

Mtegaji: kitendawili?

Mtegewa: tega!

Mifano

- Askari mlangoni		kufuli
- Nameza sisishi		mate
- Maiti amelala akitangaza	redio
- Kila mtu hunipenda		pesa
- Mwanangu analilia mwituni		shoka

Tathmini:	mufti uk 222

Kkd uk 251

- Kuandika
- Barua ya kidugu

Kuwapa muundo

Mfano:

- Anwani
- Maamkizi
- Mwili
- Hitimisho

Tathmini:	mufti uk 223

**Msamiati**

**Vitate**

Vitate ni maneno yanayotatanisha wakati wa kutamkwa

Mfano

- Baa		paa
- Ndefu		ndevu
- Fahari		fahali
- Chakura		chakula
- Kalamu		karamu

Sentensi

- Tulienda baharini kuvua samaki

- Alisuka nywele zake ndefu
- Huyu ni fahali wa babu

Tathmini: mufti uk 225

Kkd uk 24-25(ziada)

**SURA YA SITA**

**Kusoma: sentensi**

Sentensi huundwa kwa neon au maneno

Kuwaongoza kusoma kwa matamshi bora kuzingatia alama za uakifishaji

Mfano

- Mvuvi alivua samaki kasha akavua nguo kuzifua
- Mzee mrefu mwenye ndefu alimwona ndovu
- Ziwa hili lina kisiwa chenye kisima
- Baba alipopata bata alimchinja

Tathmini: mufti uk 226

Kkd uk 11

**Sarufi**

**Sifa-BICHI**

Sifa –bichi hutumika kuonyesha nomino inayorejelewa si komavu

Mfano

- Ardhi mbichi
- Chakula kibichi
- Yai bichi
- Maziwa mabichi
- Samaki mbichi

Tathmini: mufti uk 228

Kurunzi uk 150

**Kusikiliza na kuongea**

**Methali**

Methali ni fungu la maneno lenye maana fiche

Hutoa mwelekezo na maonyo

Pia huburudisha

Mifano

- Asiyeskia la mkuu huvunjika guu
- Haraka haraka haina Baraka
- Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu

Tathmini: mufti uk 228

**Kuandika**

**Sentensi: wingi/ kuakifisha**

Sentensi ni fungu la maneno

Wingi ni jumla vitu zaidi ya kimoja

Mfano

- Motto Yule alianguka
- Watoto wale walianguka
- Kikombe kile kilivunjika
- Vikombe vile vilivunjika
- Mafuta yale hutumika
- Mafuta yale hutumika
- Ugali ule umeiva
- Ugali ule umeiva

Tathmini: mufti uk 229

- Msamiati
- Marudio

Kurejelea msamiati tofauti kama vile

- Mavazi
- Shambani
- Watu na kazi zao
- Wanyama
- Viungo vya mwili

Mfano

- Kuona mambo usingizini ni? ---------------------
- Kuvuta chuchu za ng’ombe ili kutoa maziwa ni? ----------------------
- Kuwa mginjwa-----------------------------------------

Kuwapa wanafunzi zoezi

Tathmini: mufti uk 230’ 231

Kurunzi uk 117

**SURA YA SABA**

**KUSOMA**

Ufahamu: chura

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu:

a. mwalimu pamoja na wanafunzi wakichambua na kueleza fani
b. mwanafunzi wasome kwa kupokezana mmojammoja
c. Kusoma kimyakimya

Tathmini: mufti uk 234

**Sarufi**

**Vivumishi vya idadi halisi**

Vivumishi vya idadi hutumika kutupa idadi au rakamu au jumla halisi ya nomino

Mfano

- Walimu 11: kumi na mmoja
- Vikombe 2: viwili
- Miti 17: kumi na saba
- Vyura 5: watano
- Karatasi 12: kumi na mbili

Tathmini: mufti uk 236

Kurunzi uk 161

**Kusikiliza na kuongea**

**Marudio: methali**

Methali ni fungu la maneno lenye maana fiche

Mfano

- Adui mpende
- Motto umleavyo ndivyo akuavyo
- Macho hayana pazia

Kuchambua picha na kuzitaja

Kuandika majina

Tathmini: mufti uk 236-237

Kkd uk 160

**Kuandika**

**Mtungo**

Mtungo ni kihasho au kifungu chenye mapengo

Mapengo hujazwa kwa neon mwafaka

Tathmini: Kurunzi uk 110

**Msamiati**

**Marudio ya msamiati**

Kurejelea msamiati tofauti

Mfano

- Viumbe na makao
- Saa
- Nyuni
- Rangi
- Ugonjwa
- Hospitalini
- Dira
- Mavazi

Mfano

- Ukivunja yai utaona rangi ya majano
- Wageni wameketi sebuleni

Tathmini: kkd uk 170

kkd uk 172

**SURA YA NANE**

**Kusoma**

Matumizi ya kamusi

Kuwaelezea wanafunzi maneno yalivyopangwa kwenye kamusi

Kuwaongoza kusoma na kutamka maneno

Wapange maneno kama yatakavyotokea kwenye kamusi

Tathmini: mufti uk 241

**Sarufi**

**Vivumishi vya idadi ya kuonyesha nafasi**

Hivi huonyesha nafasi ya nomino katika orodha ya nomino

Mfano

- Wa kwanza
- Wa tano
- Wa mwisho
- Wa saba
- Wa nne
- Wa kumi na mbili
- Wa kumi na tisa
- Wa thelathini

Sentensi

- Mgeni wa tano amewasili
- Nilikuwa wa kwanza darasani

Tathmini: mufti uk 243

Kkd uk 170

**Kusikiliza na kuongea**

**Mjadala**

Mjadala ni mazungumzo yanayohusu kutoa hoja kwa pande mbili

Wagawe kwa vikundi

Washirikishe kutoa hoja

Tathmini: hoja za pande zote mbili

**Kuandika**

**Mtiririko: kifungu**

Washirikishe kupanga vifungu kuunda kifungu kinachoeleweka

Washirikishe kusoma kwa sauti

Tathmini: mufti uk 243

**Msamiati**

**Marudio**

Kurejelea msamiati tofauti

Mfano

- Siku za juma
- Miezi nyakati
- Mavazi
- Ukoo
- Ngege
- Wanyama

Waongoze kupanga

Mfano

Tai, kipanga, kunguru: ndege

Mazoezi ya ziada: kkd uk 186

**SURA YA TISA**

**Kusoma**

Ufahamu: kwaheri ya kuonana

Kuchambua picha

Kuchambua msamiati na kueleza maana

Kutunga sentensi

Kusoma ufahamu:

a. mwalimu pamoja na wanafunzi wakichambua na kueleza fani za lugha
b. kuteua mwanafunzi mmojammoja
c. mwanafunzi asome kimyakimya

Tathmini: mufti uk 247

**Sarufi**

**Uakifishaji: marudio**

Kueleza alama za uakifishaji kama:

- Kikomo (.)
- Koma (,)
- Hisi (!)
- Kiulizi (?)
- Kistari kifupi (-)
- Herufi kubwa

Tathmini: mufti uk 247

Kkd uk 177

**Kusikiliza na kuongea**

**Wimbo: maisha mema**

Wimbo ni kifungu cha sentensi chenye mapigo maalum

Chambua picha

Kuimba wimbo

Tathmini: mufti uk 248

Kusikiliza wanafunzi

**Kuandika**

**Hati**

Hati ni mwandiko

Mfano

Kwaheri ya kuonana

Ninawaaga tuonane baadaye

Tuwe watoto wema

Maisha mema twataka

Tunawashukuru walimu wetu

Tathmini: mufti uk 249

**Msamiati**

**Marudio**

Rejelea msamiati tofauti kama:

- Jikoni
- Magonjwa
- Wanyamapori
- Mavazi
- Ndege

Sentensi

Birika, seredani, bilauri, uteo: vifaa vya jikoni

Tathmini: mufti uk 249

Mazoezi ya ziada: mufti uk 250

Kkd uk 194

# MUHULA WA TATU

# INSHA

## BARUA YA KIRAFIKI/ KIDUGU

Barua ni maandishi yaliyo na ujumbe maalum yanayopelekewa mtu mwengine

Huwasilishwa kwa njia ya posta au kwa mkono

**Sababu ya kuandika barua ya kirafiki**

- Kujulia hali
- Kupashana taarifa kuhusu hali zao
- Kuonyana na kuomba misaada ya kidugu
- Kupashana taarifa za kimaendeleo

**Sifa za barua ya kirafiki**

- Huwa na anwani moja ya mwandishi
- Kiwango cha lugha si lazima kiwe rasmi
- Lugha hutumiwa kulingana na umri

**Anwani ya mwandishi**

- Jina la mwandishi
- Sanduku la p;osta
- Mji wa mwandishi
- Tarehe ya kuandika

Mwinyi Bokoko,

S.L.P 512,

Nakuru.

Juni 2, 2015.

**Mapambo**

Ni matumaini yangu kuwa u mzima kama kigongo cha mpingo

Nimepata afueni baada ya kuugua homa ya matumbo

Shikamoo shangazi, mjomba, mama, baba au kaka

Ni matarajio yangu kuwa u buheri wa afya

Ningependa kukufahamisha kwamba niliwasili salama salmini

Kilichonivuta zaidi ni kuchukua muda wako kunitembeza mjini/ kijijini/ ziwani/ sokoni

Sitaki kukuchosha sana kwa waraka mrefu

Wasalimie marafiki zetu na uwaambie tunawatakia kila la heri

Wapashe salamu zangu wote wanaonifahamu

Natumai utaniandikia ukinijulisha mengi ya huko mjini

**Tashbihi**

- Pendana kama chanda na pete
- Fuatana kama zinduna na ambari
- Pana kama uwanja wa ahera
- Hakika kama mauti
- Maridadi kama mbega
- Chafu kama fungo
- Adimika kama wali wa daku
- Julikana kama pesa
- Tembea vizuri kama njiwa

**Tanakali za sauti**

- Furaha mpwito mpwito/ riboribo
- Anguka topeni tapwi
- Jifunika gubigubi
- Nyooka twaa
- Cheka kwa kwa kwa
- Jaa kochokocho
- Kulala fofofo
- Giza totoro
- Lala kifudifudi

**Nahau**

- Tambo la mtu
- Barafu wa moyo
- Pigwa na kibuhuti

- Kumpa mtu nyama ya ulimi
- Kumshika mtu miguuni
- Tupa jongoo na mti wake
- Kicheko cha aiskrimu
- Kunokodolea macho
- Miondoko ya jiwa
- Kiuno chake cha nyigu
- Wakafua dafu
- Maji kuzidi unga

**Takriri**

- Marafiki wa kufa kuzikana
- Bure bilashi
- Kwa heri na shari
- Ima fa ima
- Dawa wala kafara
- Udi na ambary
- Dhahiri shahiri
- Kufa kupona
- Buheri wa afya

**Methali**

- Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
- Mvumilivu hula mbivu
- Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki
- Kidole kimoja hakivunji chawa
- Samaki mkunje angali mchichi
- Kipendacho moyo ni dawa
- Pa moyo pa mtima
- Mchumia juani hulia kivulini

**Mwisho wa barua**

Tunamalizia kwa matumaini ya kuonana na mwandikiwa, kumtakia heri au kumwomba ajibu

Mifano ya tamati

- Ni mimi wako wa mtimani
- Wako wa chanda na pete
- Ni mi mi muhibu wako
- Ni mimi mwanao

- Ni rafikiyo wa kufa kuzikana

**INSHA YA MAELEZO AU WASIFU**

Hii ni insha inayotoa maelezo kuhusu jambo, mahali au kitu Fulani

Insha hii hueleza, huarifu, huburudisha na hutahadharisha

Mwandishi asiandike chini ya hoja sita

Tumia viunganishi unapounganisha mawazo katika aya au unapoanza aya

**FAIDA ZA MITI**

Miti ni mimea yenye shina gumu, matawi na mizizi inayoshikilia miti

Kuna aina mbalimbali za miti kama vile mikaratusi, mpingo, mkuyu, mbuyu, nk

**Miti huvuta mvua**

Huvuta mvua na huzuia nchi kubadilika kuwa jangwa

Mvua huimarisha kilimo/ zaraa

Kilimo uti wa mgongo nchini

**Miti hutupa dawa**

Kuna baadhi ya miti mashina au matawi yake hutumika kama dawa

Maradhi kama malaria, kifua kikuu, homa ya matumbo hupata tiba kutokana na miti kama vile mwarobaine

**Miti hutupa hewa safi**

Kwa kweli miti ni uhai

Miti hutupa hewa safi

Bila miti hatuwezi kuwa uhai

**Makao ya wanyama**

Wanyama huishi mwituni/ msituni

Wanyama kama nyoka,chui, samba,  na ndege huishi mitini au kwenye pango

Wanyama huvuta watalii nchini

Nchi hupata pesa za kigeni

**Huzuia mmomonyoko wa udongo/ mchanga**

Huzuia mmomonyoko wa udongo

Mizizi hushika mchanga kuzuia usibebwe na maji

Huzuia upepo ambao pia waweza kubeba mchanga

**Hutupa chakula/ matunda**

Baadhi ya miti kama machungwa, mlimau, mipera, mipaipai hutupa matunda

Matunda hutupa nguvu

Bila nguvu hatuwezi fanya kazi

**Miti hutupa mbao kuni na makaa**

Nyumbani tunapika kwa kutumia makaa au kuni

Bila makaa au kuni hatuwezi pika

Miti hutupa mbao zinazotumiwa kutengeneza samani

Mifano ya samani ni makochi, kabati, meza, madawati, vibago na vigonda

**Chanzo cha mito**

Mito huanzia misituni

Ukikata miti utasababisha kukauka kwa mito

Miti ni uhai

Mifano ya mito ni Tana, Athi, Malewa nk

Mito hutupa maji ya kunyunyizia mimea wakati wa kiangazi

**Methali**

- Penye miti hapan wajenzi
- Maji hufuata mkondo
- Maji ni uhai

**NCHI YANGU**

Nchi yangu inaitwa Kenya

Iko katika bara la Afrika, eneo la Afrika mashariki

Linaongozwa na rais ambaye huchaguliwa na wananchi kote nchini baada ya kipindi cha miaka mitano

Nchi yangu ilipata uhuru kutoka kwa Uingereza mnamo mwaka wa 1963

Tukikuwa tukiongozwa na wabeberu waliotutesa sana

Mababu zetu ndio waliopigania uhuru

**Marais**

Nchi yetu tumeongozwa na marais watatu na sasa wan ne ndiye yu mamlakani

Nchi yetu ina raia wengi(milioni arubaine)

Nchi yetu ina mali mengi kama vile wanyama wa pori, madini, maziwa na mashamba yenye rutuba

Uti wa mgongo nchini ni kilimo/ zaraa

Tunazingirwa na majirani mbalimbali mfano Tanzania, Uhabeshi, Uganda, Sudan, Bahari ya hindi na Somalia

Tuna uhusiano mwema dhidi ya majirani wetu

Nchi yetu huuza bidhaa mbalimbali kama vile majani, kahawa, maziwa na pareto katika nchi za ughaibuni

Tunanunua mashine, erektroniki, mbolea na mafuta kutoka nchi nyingine

Watalii huzuru nchi yetu angaa kuwaona wanyama pori, maporomoko ya ardhi na mandhari yanayovutia

Utalii huiletea nchi yetu pesa za kigeni

Nchini kuna shule nyingi za msingi , upili na vyuo vikuu

Nchi yetu imegawanywa katika kaunti arobaini na saba

Sisi huishi kaunti ya Nakuru

Nchi yetu inafahamika kote duniani kutokana na riadha na michezo mbalimbali

Nchi yetu ina maendeleo makubwa ya miundo msingi kama vile barabara, reli na Nyanja za ndege

**Funzo**

Tunastahili kuwaripoti wanaoshiriki katika vikundi vya ugaidi

Tuwe wazalendo dhabiti na tuunge maendeleo mkono

**INSHA YA HADITHI**

Hadithi pia huitwa ngano au hekaya

Hadithi ni masimulizi ya matukio yaliyopita

Huwa wakati mwingi ni visa vya kubuni

Huwa na sehemu tatu

**Mwanzo**

Huchukua mwanzo maalum

Mfano

- Hadithi hadithi, hadithi njoo…………………………
- Hapo zamani za kale…………………
- Hapo kale paliondokea……………………..
- Hapo miaka na mikaka………………………..
- Hapo enzi za babu yanguBahu palikuwa……………………..
- Hapo jadi na jadudi palikuwa……………..

**Mwili**

Kisa chenyewe hutolewa na kueleza matukio

Mfano

- Kwanini sungura ana maskio marefu
- Kwanini kombe ana magamba

Mapambo mengi hutumika

**Mwisho**

Hutoa funzo mtu alipatalo kutokana na hulka za wahusika

Mfano

- Hapo ndipo nikaamini kwamba njia ya mwongo ni fupi
- Hapo ndipo nilipojua kwamba majuto ni mjukuu na huja kinyume
- Hiyo ndiyo maana chui huchechemea hadi leo atembeapo

**Tashbihi**

Shingo kama twiga

Eusi kama lami/ mpingo

Mbio kama swara

Fupi kama mbilikimo

Nuka kama beberu/ kidonda

**Methali**

Asiyeskia la mkuu huvunjika guu

Subira huvuta heri

Ahadi ni deni

Kidole kimoja hakivunji chawa

**Tanakali**

Alitiririkwa na damu tiriri

Machozi yalimdondoka ndondondo

Walishimba ndi

Waliangua kicheko kwa kwa kwa

Aliula ule mzoga akaumaliza fyu

**Istiara**

Fisi alikuwa samba

Yule bikizee alikuwa nyundo

Alikuwa kinyonga

Kimondo alikuwa na ulimi mrefu

Alipokaidi mzee alikuwa kondoo

**Sentensi**

Siku ile wanyama walikula wakashimba ndi

Samba Yule mzee alikuwa mweusi kama lami

Hapo ndipo sungura akaja kujua kwamba siku za mwizi ni arobaini

Alipanda migomba, minazi, mipareto na mihindi. Alifanya bidii za mcwa na wenzake wakamwonea kijicho

**INSHA YA KUENDELEZA**

Hapa mwanafunzi hupewa mwanzo wa insha kasha anaiendeleza. Ni bora kusoma na kuelewa kabla ya kuanza kuandika

Mambo muhimu ya kuzingatia

Kuwa na mpango maalum baada ya kusoma

Kuteua msamiati unaofaa

Kuchagua mapambo ainati

Kuandika insha yenye mvuto

Kupitia kazi yako baada ya kuandika

**Mfano wa insha**

Tulizidi kuyapuuza makanyo yam zee Kombo. Alikuwa akitushauri kwamba tusiogelee katika mto kibisi. Nasi tukayatia masikio nta. Siku moja…………………………………………………………………………………………………………

**Mapambo**

Tulifurahia maji na kushindana kwa uogeleaji

Galacha wa kuogelea alitutia hamasa ya kuogelea zaidi

Tulitoka mmoja mmoja baada ya mwengine na kurudi majini

Ghafla bin vuu rafiki yangu alivua nguo na kujitosa majini

Baada ya muda mrefu, tulitoka majini na kujilaza kwenye mawe kama mjusi

Tulipiga kamsa zilizowazindua wakulima

Baba aliposkia habari hizo alichemka nyongo sana

Siku iliyofuata tulimtembelea rafiki yangu hospitalini alikolazwa

Tulipowasili tulikabiliwa kwa maswali mengi

Machozi yalitundondoka nyusoni/ machoni lakini yakimwagika hayazoleki

Mawazo yaliduru kichwani kama pia

Tulicharazwa viboko tukalia mpaka machozi yakaghairi kutoka

Tuliachwa tukisinasina kama watoto wadogo

**Nahau**

- Piga mbizi-ogelea
- Kupiga soga
- Maji mafu
- Kucheka kama radi
- Kupigwa dhoruba na maji
- Kuelea juu ya maji
- Kupiga kamsa/ ukwenzi/ usiahi
- Kumeza matunda ya maji
- Pigwa bumbuazi
- Kuchungulia kaburi
- Kuzama zi
- Kufa moyo
- Kupiga moyo
- Kupiga kachombo

**Tanakali za sauti**

- Anguka kacha/ tang/ tifu/ pu
- Tumbukia chubwi
- Demka dem dem
- Rowa rovu rovu
- Teleza prrrr

- Zama zi
- Koma kome kome
- Lia kwi kwi kwi
- Jaa furi furi

**Tashbihi**

- Epesi kama usufi
- Tumbo kama kiriba
- Iga kama kasuku
- Ringa kama tausi
- Lazima kama ibada
- Fura kama hamira
- Dhaifu kama mkufu/ mgonjwa wa satura
- Lala kama mfu
- Mrefu kama komanzi
- Ogelea kama samaki
- Kipofu kama jongoo
- Simama wima kama dandalo
- Mwoga kama kunguru
- Eupe kama joya

**Taswira jozi**

- Udi na uvumba
- Maji na mafuta
- Shiba na njaa
- Katika jua na mvua
- Shangwe na hoihoi
- Ficha na kufichua
- Heri na shari
- Kufa na kupona
- Uta na upote
- Balaa na belua
- Zogo na zahama
- Mapana na marefu
- Pua na mdomo
- Tenge tahanani

**Methali**

- Sikio la kufa halisikii dawa
- Mwenye pupa hadiriki kula tamu
- Kelbu/ mbwa hafi maji aenapo ufuko
- Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe
- Cha kuzama hakina rubani
- Asiyesikia la mkuu hununjika guu
- Msiba wa kujitakia hauna kilio
- Mwimba wa kuchoma hauambiwi pole

Tanbihi: wanafunzi waandike insha ya kuendeleza inayohusiana na kuogelea majini

**AJALI BARABARANI**

Ajali ni tukio lenye madhara linalotokea ghafla

Husababisha maafa au majeraha

Mwanafunzi anahitajika kusimulia kisa kinachohusisha magari, baiskeri au pikipiki katika ajali

**Mwanafunzi azingatie**

Ulikuwa wakati gani ajali ilipotokea

Alikuwa akielekea wapi aidha kwa garia au kwa miguu

Ajali yenyewe ilihusisha nini

Ni nini kilichofuatia baada ya ajali hiyo:

- hisia za wahusika
- kuagiza msaada kwa majirani au polisi

**Msamiati**

Kuamka jogoo la kwanza

Demka/ rauka majogoo

Piga mswaki

Koga hamamuni kwa dodoki/ sifonga

Kujikwatua kwatukwatu/ kujipamba pambepambe

Valia libasi zilizongaa kama mbalamwezi

Gari kutiwa moto na dereva/ mshika usukani

Kungoa nanga

Kaa karibu na dirisha kujionea mandhari yaliyovutia

Kujifunga mkanda wa usalama

Piga soga/ gumzo/ porojo

Mwendo wa kasi kama duma/ risasi/ umeme

Gurafu

Matuta

Yumbayumba

Shindwa kudhibiti gari

Gongana dafrau/ ana kwa ana

Bingirika bingiribingiri

Vigae vigae

Damu kutiririka tiriri

Vilio vilienea kote

Machozi ya majonzi

Machozi yalipukurika puku puku

Biwi la simanzi lilitanda kote

Kuwanusuru manusura

Kulilia uhai wao

Kupelekwa Thieta

Kufungwa Plasta

Wafu kupelekwa mochari/ ufuoni/ makafani

Mkasa huo utasalia katika kumbukumbu zangu

Mahututi

**Methali**

Haraka haraka haina Baraka

Mwenda pole hajikwai

Kawia ufike

Ajali haina kinga wala kafara

Polepole ndio mwendo

Ajali haijali